


BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI



TAARIFA KWA UMMA UDAHILI WA STASHAHADA NA ASTASHAHADA KATIKA VYUO MBALIMBALI KWA MUHULA WA MACHI KWA MWAKA WA MASOMO 2021/2022

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ni chombo kilichoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Sura ya 129 ili kusimamia na kuratibu utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo katika vyuo vya Elimu ya Kati. Jukumu mojawapo la Baraza ni kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa katika Vyuo vya Ufundi nchini yanakidhi vigezo na ubora unaohitajika katika soko la ajira ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Baraza linao wajibu wa kuratibu udahili wa wanafunzi kwenye Vyuo na kozi/programu zinazotambulika na mamlaka husika.

Dirisha la udahili kwa muhula wa Machi kwa mwaka wa masomo 2021/2022 lilifunguliwa tarehe 15 Januari, 2021 hadi tarehe 20 Februari, 2021. Waombaji wa kozi za Stashahada na Astashahada walituma maombi ya kudahiliwa katika Vyuo mbalimbali. Baada ya dirisha la udahili kufungwa, Vyuo vilifanya mchakato wa maombi ya udahili na kuchagua waombaji wenye sifa. Waombaji waliochaguliwa waliwasilishwa NACTE kwa ajili ya uhakiki kuanzia tarehe 22 mpaka 27 Februari, 2021.

Jumla ya waombaji **7,934** waliochaguliwa kujiunga na programu mbalimbali zinazotolewa na Vyuo waliwasilishwa NACTE kwa ajili ya Uhakiki. Kati ya hao, waombaji **7,197** (91%) wamekidhi vigezo vya kujiunga na programu walizochaguliwa na waombaji **737** (9%) hawana vigezo vya kujiunga kwenye programu walizochaguliwa. Majibu ya Uhakiki huu yametumwa Vyuoni tayari.

Waombaji wote waliowasilishwa NACTE kwa ajili ya Uhakiki na kuwa na vigezo vya kujiunga na programu walizochaguliwa wametumiwa ujumbe na msimbo (*Code*) kupitia simu na barua pepe walizowasilisha wakati wa kuwasilisha maombi ya udahili. Msimbo huo uwasilishwe chuoni kwa ajili ya usajili na uhakiki kupitia tovuti ya Baraza (www.nacte.go.tz).

Aidha, maombi ambayo hayakukamilika kutokana na sababu mbalimbali, Vyuo vimepewa nafasi ya kurekebisha kasoro hizo kuanzia tarehe 8 hadi 12 Machi, 2021. Wito unatolewa kwa Vyuo kuitumia nafasi hiyo kikamilifu na kufanya marekebisho hayo kwa wakati kwakuwa hakutakuwepo na nafasi nyingine ya marekebisho kwa muhula wa Machi 2021/2022.

Masomo kwa waliochaguliwa yataanza rasmi kuanzia tarehe **1 Aprili, 2021**. Hivyo, wazazi na umma kwa ujumla waepuke kutapeliwa na wale wanaodai kwamba masomo yameanza kabla ya tarehe hiyo.

IMETOLEWA NA:
OFISI YA KATIBU MTENDAJI
BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI (NACTE)
TAREHE: 05/03/2021